# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA KUMI NA TANO

**30 APRILI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA KUMI NA TANO – TAREHE 30 APRILI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA MADINI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati

kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## III. MASWALI:

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**182. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Barabara za lami katika Mji Mdogo wa Karatu.

**183. MHESHIMIWA ALEKSIA ASIA KAMGUNA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Barabara za Wilaya ya Malinyi kwa kiwango cha lami.

**184. MHESHIMIWA NEEMA GERALD MWANDABILA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza kutoa Mshahara kwa Madiwani ili waweze kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

**185. MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL MKUNDI (UKEREWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka Watumishi wa Afya wa Kike wa kutosha - Ukerewe ili kulinda haki ya kijinsia ya Mtoto wa Kike.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**186. MHESHIMIWA MUSSA OMAR SALIM (GANDO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, lini ahadi ya Serikali ya kuzuia maji chumvi kuingia katika Bonde la Mpanja Gando itatekelezwa.

**WIZARA YA NISHATI:**

**187. MHESHIMIWA ABDALLAH JAFARI CHAUREMBO (MBAGALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini kukatika umeme mara kwa mara Kata za Chamazi, Mianzini, Kilungule, Charambe, Mbagala, Kiburungwa na Kijichi Mbagala Kuu kutaisha.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**188. MHESHIMIWA ROBERT CHACHA MABOTO (BUNDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itajenga Makao Makuu ya TANAPA katika Halmashauri ya Mji wa Bunda.

**WIZARA YA KILIMO:**

**189. MHESHIMIWA DAIMU IDDI MPAKATE (TUNDURU KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga maghala ya kuhifadhia mazao Vijijini.

**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**190. MHESHIMIWA TIMOTHEO PAUL MNZAVA (KOROGWE VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itapeleka Mawasiliano ya Simu kwenye Kata za Mkalamo, Magila, Gerezani na Kalalani – Korogwe Vijijini.

**WIZARA YA MAJI:**

**191. MHESHIMIWA SEIF KHAMIS SAID GULAMALI (MANONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itatenga fedha ili Wananchi wa Kata za Igoweko, Uswaya na Tambalale – Manonga wapate maji ya Ziwa Victoria.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**192. MHESHIMIWA MWATUM DAU HAJI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti Mimba za Utotoni Nchini.

**WIZARA YA UJENZI:**

**193. MHESHIMIWA ATUPELE FREDY MWAKIBETE (BUSOKELO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Barabara inayounganisha Jimbo la Busokelo na Mbeya yenye Km 28 itajengwa ili Wananchi wasisafiri umbali mrefu kupitia Suma hadi Katumba.

**194. MHESHIMIWA MASACHE NJELU KASAKA (LUPA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Selikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya kuanzia Makongorosi hadi Mkiwa.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**195. MHESHIMIWA SUMA IKENDA FYANDOMO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itapeleka Magari kwenye Vituo vya Polisi Mkoa wa Mbeya.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**DODOMA** **BARAKA I. LEONARD**
**30 APRILI, 2025** **KATIBU WA BUNGE**

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA